# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

## TOLEO MAALUMU LA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NDANI YA MANISPAA YA KIGAMBONI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 4 YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA







# SEKTA YA AFYA

## UJENZI WA KITUO CHA AFYA MJIMWEMA

Kata ya Mjimwema iinajumla ya zahanati tatu (03) zilizopo Mtaa wa Maweni, Ungindoni na Mtaa wa Kubugumo ambazo zinahudumia wakazi wapatao 54,859.

Kutokana na sera ya nchi ya kila kata iwe na kituo cha Afya, kata ya Mjimwema inakujenga kituo cha Afya kwa njia ya gorofa katika mtaa wa Mjimwema eneo la Kisota na kuiitwa jina la **MAMA SAMIA HEALTH CENTER.**

Mradi huu wa ujenzi wa Kituo hiki cha Afya ( Mama Samia Health Center) uliibuliwa na Wananchi wa Kata ya Mjimwema kwa kuwa maeneo haya hayana huduma ya Afya na fedha za utekelezaji wa mradi huu zinatolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kutokana na makusanyo ya Mapato ya ndani ya halmashauri, hivyo fedha za ujenzi wa mradi huu ziilizotengwa kwa awamu ya kwanza kumaliza hadi sakafu ya kwanza ambayo ni shilingi milioni miatisa (900,000,000/-) kutokana na hali ya makusanyo ya halmashauri na hadi sasa kiasi cha shilingi milioni 434,000,000.00 zimesha tolewa na halmashauri

Utekelezajai wa mradi huu unafanywa kwa njia ya Nguvu kazi (Force akaunt) na kwa sasa utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 35 ya utekelezaji kwa awamu hii ya kwanza, ambayo ilianza Tarehe. 18/04/2024 na hatua iliyofikiwa kwa sasa



*MUONEKANOWA JENGO LA WODI YA WAKINA MAMA WAJAWAZITO KATIKA HOSPITALI YA VIJIBWENI*

ni umaliziaji wa Vitako vya msingi, Vishina vya Nguzo,ujenzi wa matofari ya msingi kurudishia udongo,kuandaa umwagaji wa jamvi na kiasi ambacho kimekwisha tumika ni shilingi 433,872,040.00 na zilizobaki ni shilingi 127,960.00

Kutokana na ukubwa wa mradi huu, kabla ya kuanza ujenzi zilifanyika kazi tano (05) za msingi na ambazo zilikamilika wa asilimia 100 zilijumuisha Upimaji wa Udongo, Ufanyaji wa athari za mazingira (EIA) Uchimbaji wa kisima, Ujenzi wa banda ya kuhifadhi Vifaa vya ujenzi, pamoja na ujenzi wa Vyoo.

Mradi huu utakapokamilika unatarajia kutoa huduma za Dharula, wagonjwa wa nje(OPD) Huduma za kulazwa (IPD) Mama na Mtoto (RCH), huduma za uzazi na Upasuaji,huduma za kinywa na Meno, huduma za mionzi, Maa-bara na huduma nyingine. Aidha mradi huu utawahudumia wakazi wa Kata ya Mjimwema hususani Mtaa wa Mjimwema, Ungindoni, Maweni na wananchi wa maeneo ya jirani.

# MIFUGO NA UVUVI

## UJENZI WA MACHINJIO YA MIFUGO ENEO LA BAMBA

Manispaa ya Kigamboni .ina jumla ya ng'ombe **21,465**, mbuzi **9,552** na kondoo **3,811** .Pamoja na kuwa na idadi hii kubwa ya Mifugo, nyama inayoliwa inazalishwa kutoka kwenye machinjio zilizoko nje ya Manispaa ya Kigamboni na hivyo kutoa mwanya kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kuchinjia maeneo yasiyo rasmi na kuhatarisha afya ya walaji.

Kwa sababu hizo Manispaa iliona haja ya kujenga machinjio kwa lengo la kuboresha afya za wakazi wake, kuongeza mapato ya Halmashauri lakini pia kuwa kituo cha awali cha kubaini magonjwa mbalimbali ya mifugo.

lengo la Mradi huu ni Kuboresha lishe kwa kuhakikisha kuwa jamii inapata nyama safi na salama, Kuwa kituo cha awali cha kubaini magonjwa mbalimbali ya mifugo, Kuongeza pato la Halmashauri na kutoa ajira kwa Wananchi wa Kigamboni

mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 03/05/2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025. na Mpaka sasa utekelezaji umefanyika kwa asilimia 80

Machinjio hii itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 50-80 na mbuzi 80-120 kwa siku hivyo kurahisisha upatikanaji wa nyama katika Manispaa manufaa ya mradi huu ni Kuongeza mapato ya Halmashauri, Uhakika wa usalama wa nyama utakuwa rahisi hivyo walaji kupata nyama safi na salama, Ajira kwa wananchi kwenye mnyororo mzima wa thamani na kupunguza gharama kwa wafanyabiashara wa Kigamboni



***Muonekano wa mbele wa Machinjio ya kisasa ya Bamba***



*Muonekano wa Ndani wa Machinjio ya kisasa ya Bamba*

# SEKTA YA ELIMU

## Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Mbutu

Kata ya Somangila ni miongoni mwa Kata 9 zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni. Kata hii inaundwa na jumla ya Mitaa 13.

Katika kuhakikisha huduma ya Elimu inasogezwa karibu kwa Jamii na Kila Mtoto anapataa nafasi ya kwenda Shule,

Kata ya Somangila, ilipokea fedha kiasi cha Tsh Mil 350,000,000/= kutoka Serikali kuu kupitia mradi wa SEQUIP lengo likiwa ni kusogea huduma ya elimu kwa Wananchi kwa kujenga shule mpya ya Sekondari ya Mbutu

ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari ya Mbutu. ulianza rasmi tarehe 02/03/2024 ukihusisha majengo 6 ambayo ni :-

I. Jengo la Utawala
II. Jengo la Madarasa 2
III. Jengo la Madarasa 2 na Ofisi
IV. Jengo la maabara ya Kemia na Baiolojia.
V. Jengo la matundu 4 ya vyoo vya Wavulana
VI. Jengo la Matundu 5 ya vyoo vya Wasichana.

Hatua ya ujenzi iliyofikiwa kwa sasa ni umaliziaji ( Finishing).

Shule hii itafanikiwa kupunguza umbali wa Wanafunzi ambao wamekuwa wakisafiri kwa umbali wa zaidi ya Kilomita 3 kufuata huduma ya elimu

Mradi pia utaongeza wigo wa upatikanaji wa Elimu kwa Wananchi wa Manispaa ya Kigamboni .



*Miundombinu ya Jengo la vyumba viwili vya Madarasa katika Shule ya Sekondari ya Mbutu*



*Miundombinu ya Jengo la Madarasa na Ofisi katikati Shule ya Mbutu*



*Miundombinu ya Jengo la Maabara ya Biolojia Shule ya Mbutu*

# SEKTA YA ELIMU

## Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari ya Mkamba

Katika kuhakikisha huduma ya Elimu inasogezwa karibu na Jamii na Kila Mtoto anapataa nafasi ya kwenda Shule, Kata ya Kisarawe ii ilipokea kiasi cha Tsh : 528,998,425.00 kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa SEQUIP kwaajili ya ujenzi wa shule Mkamba.

Lengo la kuanzisha shule hiyo ni kuhakikisha Elimu ya Sekondari inawafikia wanafunzi waliomaliza kidato cha Saba. ujenzi wa Shule ulianza rasmi tarehe 01/10/2024. ukihusisha Jengo la;-

I. Ujenzi jengo la utawala
II. Jengo la Madarasa mawili na Ofisi
III. Ujenzi wa jengo la maabara ya kemia na biologia na Fizikia
IV. Ujenzi wa jengo la Makataba
V. Ujenzi wa jengo la Tehama
VI. Ujenzi jengo la matundu matano vyoo vya wasichana na kichomea taka
VII. Ujenzi jengo la matundu manne vyoo vya wavulana .

hatua ulipofikia mradi kwasasa ni kupau, kufunika mashimo ya maji takaMradi pia utaongeza wigo wa upatikanaji wa Elimu kwa Wananchi wa Manispaa ya Kigamboni.



*Jengo la Utawala Katika Shule ya Mkamba*



*Muonekano wa Jengo la TEHAMA (Kompyuta room), Shule ya Mkamba*



*Muonekano wa vyumba 2 vya Madarasa na Ofisi 1, Shule ya Mkamba*

# SEKTA YA BARABARA
# USIMIKAJI WA TAA ZA BARABARANI

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kasim Majaliwa alipotembelea Wilaya ya Kigamboni katika ziara yake aliyoifanya tarehe 06/10/2024 alitoa maelekezo kwa uongozi wa Wilaya ya Kigamboni kuhakikisha wanaweka taa za Barabarani kwenye maeneo muhimu yanayofanya shughuli mbalimbali za Kibiashara ili wananchi waweze kuendesha Biashara zao kwa Muda wote.

Katika kutekeleza agizo hilo Manispaa ya Kigamboni kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya iliweza kufanya utambuzi na kubaini maeneo muhimu ya kibiashara kwa nyakati zote na kufanikiwa kuweka taa katika maeneo 7 ikiwemo eneo,

1. Soko la Kibada ambapo taa 17 zimefungwa
2. Eneo la Feri karibu na Stendi zimefungwa taa 4.
3. Mwemberado lilopo eneo la Mikadi zimefungwa taa 12
4. Eneo la Fukwe ya Mikadi zimefungwa taa 12
5. Eneo Dege zimefungwa taa 6
6. Tungi zimefungwa taa 11
7. Eneo la maweni center taa 8

Na kufaya taa zilizofungwa katika maeneo hayo kufikia 67 kuwekwa katika maeneo hayo. Uongozi wa Wilaya ya kingamboni unatoa wito kwa Wanachi wote kutunza na kuzilinda taa hizo ili shughuli za uzalishaji ziendelee kufanyika kwa maasaa yote



*Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kasim Majaliwa akizungumza na wananchi katika uwanja wa Mjimwema*



*Muonekano wa Taa za barabani katika Barabara ya Maweni-Tungi*



*Miundombinu ya Jengo la Madarasa na Ofisi katikati Shule ya Mbutu*

# UWEZAJI WA WANANCHI KIUCHUMI
# UGAWAJI WA VITAMBULISHO VYA WAJASIRIAMALI




Katika kuhakikisha Serikali inawainua wananchi kiuchumi Mkuu wa wilaya ya kigamboni Mhe. Halima Bulembo alizindua rasmi vitambulisho vya kidijitali kwa wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama Machinga katika hafla fupi iliyofanyika katika uwanja wa Tungi mnadani

akizungumza wakati wa uzinduzi huo Mhe. Halima Bulemboametoa wito kwa wafanyabiashara hao.Kuendesha shughuli zao katika maeneo rasmi ikiwemo Soko la kibada ili waweze kutambulika



*Mama lishe akipokea kitambulisho cha kidijitali cha mfanyabiashara ndogo ndogo (Machinga)*

Na kupata huduma zinazolingana na shughuli zao.

Aidha amesema Serikali inatekeleza jukumu la kuwawezesha wafanyabiashara kupitia wizara ya Maendeleo ya jamii ili kuhakikisha linakuwa kiuchumi kwa kujiajiri katika shughuli mbalimbali.

Mfumo huu mpya wa vitambulisho vya kidijitali unalenga kurahisisha utambuzi na kuboresha mazingira




ya biashara na kuwaunganisha wajasiriamali katika maeneo yao kupitia fursa mbalimbali za kiuchumi .

Aidha ili kujisajili na kupata kitambulisho hicho muombaji anapaswa kuwa na namba ya kitambulisho cha taifa (NIDA) barua ya utambulisho kutoka ASerikali ya Mtaa na kulipia kiasi cha Tsh 20,000/= mfumo huu unatarajia kuchochea ukuaji wa uchumi kuboresha ustawi wa wafanyabiasharra ndogo ndogo ndani ya Wilaya ya Kigamboni

## MIAKA 63 YA UHURU WA TANZANIA BARA:
## ‘UONGOZI MADHUBUTI WA WANANCHI NI MSINGI WA MAENDELEO YETU’

### HABARI KATIKA PICHA







**Manispaa ya Kigamboni inamshukuru Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuleta fedha kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Sekta mbalimbali**

**‘KAZI IENDELEE”….**







**Limeandaliwa na**

**Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni**
**SLP 36009**
**Dar es Salaam**

**Chini ya**

**Kitengo cha mawasiliano Serikalini**

**Mtayarishaji**

**Joseph Semkiwa**

**Mhariri**

**Honorata Minde**

**Wapiga picha**

**Kinji Mwandika**
**Deusdedity Msemba**